Wachira Munene: Asante sana Bwana Commissioner, jina langu ni Wachira Munene. Sana sana nitaongea kuhusu chama. Mimi ndiye Chairman wa Democratic Party hapa location lakini point yangu ya kwanza ni Kenya iwe non party state, iwe partyless state. Hayo mambo ya vyama iondelewe. Tukitaka kupigania viti tunapigania tukiwa wakenya lakini sio wa DP, wa Kanu, wa nini.

Ya pili ni one man, one job, one property. Hatutaki watu wawe na mali mingi. Ikiwa ni shamba uwe na moja na iwe gazetted na uandikwe uko na hiyo moja, usikue na tano ama kumi.

Ya tatu, Kenya tuko na watu wengi sana hawana mali, hawana pesa. Tungetaka serikali yetu iwe na National Social Security Card badala ya kitambulisho ili watu wale hawana kazi wanajulikana kwa serikali na mwisho wa mwezi wanapatiwa pesa zile za National Security.

Bwana Commissioner, kwa sababu sina memorandum ningetaka uchukue hii.

Ya tano, mamlaka ya President iondolewe, iwe kidogo kama bunge itaona ile anahitaji. National days na national monuments na national heros wazingatiwe na Parliament na watu wawekwe kwa gazeti ili Kenya yetu tujue who served where and who did what. Ya mwisho, serikali ipatie wananchi wakili wa kuwatetea sana sana. Asante sana.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much Councillor, hayo ni maneno mazuri. Mary Othaya? Mary tafadhali njo haraka kama ndiwe Mary Othaya. Niwe wetaguo Mary, nukwaritie? Ni thena uriko wenaguo? Akae chini tutafafuta mtu.

Mary Othaya: Jina langu naitwa Mary Othaya wa Gatiki. Nimekuja mbele yenu kwa sababu ya maumivu na nimefurahi sana kwa sababu ya kuja. Kwa sababu nikiwa barabarani nikikuja nilisema kama ni wakati wa kuenda bunge hata mimi naweza kwenda nikatetea watoto na boma zetu kwa sababu nyumba zetu zimeporomoka.

Hapo mbeleni kanisa ilikua muhimu, ilikua inaweka watu pamoja lakini sasa nikupoteza inapoteza watu. Tunaomba serekali itusaidie kwa sababu ya watoto wetu na wazee wetu kwa sababu wazee wetu wanatupiga viboko kwa sababu wanataka kuuza mashamba ndio watafute mabibi wengine hapo. Hebu muniangalie mahali nimepigwa, mama na watoto wafukuzwe ndio wachukuwe hayo mashamba wauze na walete mabibi wengine. Ndio munaona vifo vimezidi na mimi ninasema afadhali nikufie hapo. Nikipigania uhuru wangu wa nchi yangu huyo munasikia anaitwa Kimathi ni wetu nikasema nitashika yeye kama buda yangu kwa sababu siwezi kukataa.

Tunapiga nduru hata kwa machief, machief nao ni marafiki wa wazee wetu. Tunapiga nduru sana tumelia machozi sana. Tunauliza serikali itusaidie zaidi na tunahujumiwa na watu wa ma -kanisa kwa sababu kwa makanisa wanatujalia, hana haja na roho za watu. Wacha niwa dondolee hayo. Sasa nimesema kamisa hayo sasa nime ndio inafanya mzee auze hiyo shamba. Muniangalie vizuri ndio alete gachungwa watoto wangu wamekata kupatiwa gold mine na hawakusomeshwa na pesa ziko.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Niwega hau nidagiwa. Point ya muthia.

Mary Othaya: Tunaomba serikali itusaidie na ituwekee security nyumbani mwetu kwa sababu imeharibika. Watoto wamekua machokora na wako na vitu. Serikali isaidie watoto na wamama tuwe na amani kwam vile ilivyokuwa mbeleni. Na mtu akimuweka mimba msichana awe anapewa mali kama vile ilikuwa hapo mbeleni. Mambo yawe vizuri kama hapo mbeleni. Asante.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Niwega. John Munuhe? John, I want you to only talk on those things that have not been presented. Do you have a memorandum? Okay fine.

John Munuhe: I am John Baptista Munuhe, I am a resident of Kieni Constituency, Kieni East Division. I will start with our

citizens that we have people found in almost all our urban areas who do not have anywhere to sit, they loiter and sleep in the streets. We would like our Government to take care of these people and especially removing them from the streets and find them a proper home.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Yes, that is taken.

John Munuhe: The next item I have here is that our primary schools, I mean we should revert to the old system that is 7-4-2-3 and again we should have preparatory classes integrated into primary school curriculum. That is by having properly trained teachers to take care of ages 4 and 5 and these ones should be employed by Teachers Service Commission.

There should be land ceiling and this one should go in accordance to the potentiality of a certain region. That means in high potential regions acreage should not exceed 50 acres. In less potential areas acreage should be 75. In the least potential areas the acreage should not exceed 100 acres.

The next one. All the land that is above the limit that I have stated here should be taxed and the tax accrued from this land should help buying first inputs so that we alleviate the burden on our farmers. After that, all the people displaced during the infamous tribal clashes in the years 1990 up to 1998, these people should be resettled and if possible the instigators should be put to trial because that was a very bad thing in our country and especially those who took part in the meetings of Kabsabet, Kaptet and Narok, they should be known.

There should be education standards for councillors.

Com. Bishop Bernard Njoroge: What is the standard?

John Munuhe: It should be Form four at least, Form four education.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Fine. Go to the next point.

John Munuhe: Thank you very much. Retirees who were civil servants are suffering a lot because the Government is not taking care of these people. They are spending even four to five years before they get their benefits. It should be put in place that after only three months, that is after the date of retirement, one should enjoy his or her benefits.

KBC should treat all political parties equally. Note that KBC will always report positive things on the Government party.

Com. Bishop Bernard Njoroge: That is alright we have taken that. One more.

John Munuhe: The last one. The Government should free airwaves so that our people are reached in all the parts of our country. Thank you Mr. Commissioner.

Com. Bishop Bernard Njoroge: John, unajua mambo wewe. Sawa. Joseph N'gang'a.

Joseph Nganga: Jina langu ni Joseph N'gang'a na ningependa ku comment juu ya elimu. Elimu inapaswa iwe free kutokea Standard One mpaka University.

Jambo la pili. Tuwe na Economic Council ambayo itashughulika na mambo ya kufanya taratibu na maswala ya uchumi ambao itakaliwa na wale watu ambao wana elimu ya chuo kikuu na watu wenye akili za juu. Pia upande wa agriculture tuwe wa usimamizi ya bei kama vile zamani kuwe na minimum ili iweze kushughulikia mambo ya ku-offset expenses ambazo wakulima wametumia katika kukuza zao lao. Thank you very much.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much, you have tackled the most important aspect. Thank you Joseph. Simon Wachira. Una memorandum?

Simon Wachira: Hapana, just points. Straight to the point. I am Simon Wachira, deeply concerned by the retrogressive brain drain, the dual citizenship should be recognized. There should be reached a rigid Consitution that recognizes the existence of a powerful President, a Prime Minister and two Deputy Presidents and should there be a change, then a National Referendum should be sought.

No. three. Deeply alarmed by excessive use of force the Provincial Administration should be abolished but instead strengthen the local Government.

No. four. There should be an efficient monitoring unit composed by members of the Public Investment Committee, Public Accounts Committee, Judges, Attorney General and the Office of the Ombudsman. This Committee should have power to prosecute those who misuse public offices and public funds.

No. five. Deeply disturbed by unemployment, there should be a Constitution that recognizes expatriates in subordinate roles only not just the Chief Executive officers because we have got a pool of qualified graduates who are more patriotic and loyal. The President should get 50% of the votes and finally there should be a supreme Constitution that is not selectively applied. We should not get some tribes carrying weapons in towns and go scot free while others are taken as culprits when they do so.

Leaders proved guilty beyond reasonable doubt by Public Investment Committee and Public Accounts Committee should be

forced to resign and should be prosecuted and hold no public office in the future. Thank you.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much, very important points and well said. Thank you very much Simon. Nderitu Muema?

Nderitu Muema: I am Nderitu Muema. Myself, I am having a bill which is a bit different from what we are speaking because I know and we have heard that we are at liberty. Next elections should be supervised by United Nations.

Secondly we should use voting machines. Another thing is that the President should not be above the law and he should hold a University degree and be the age of 50 years. Abolition of Provincial Administration. Cooperative Act should be abolished and nomination of MP and councillors should be abolished.

Going to Parliament, before they quit they should elect a new Electoral Commission in order to cope with what is coming. For a party to nominate a candidate, he/she should be in that party for two years and the party then should be more than two years old.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much those are very important points you have given us. Can we have Peris Muthoni Watata? Where is the interpreter?

Peris Watata: Jina langu ni Peris Muthoni Watata au Mrs. Watata. Mimi ni mkazi hapa Naro Moru katika sub location ya Kaburaini. Ni furaha yangu kubwa sana kwa vile serikali imefanya kukuja hapa tuwape maoni ya mambo tunavyona. Mimi wakati bendera ilipepea mlimani nililala hapa Naro Moru na Bwana Munyao. Kwa hivyo uhuru ulipiganiwa na Mau Mau na watoto wetu waliuwawa na walikwisha na wengine tulisikia walienda Ethiopia. Mtu ambaye anaitwa Mathenge Mirugi na hatujasikia hali yao tena. Nauliza serikali haikufurahia Mau Mau kufukuza mzungu hapa na kupata mashamba yetu sisi wenyewe? Kwa hivyo napenda kuuliza serikali, serikali si mbaya kwa sababu tunaongozwa na kijana mdogo anaitwa Nyayo na ni wa rika langu. Alizaliwa 1924 kama vile nasikia na mimi nilizaliwa 1924. Tunafurahi sana.

Kwa hivyo mtu akikimbia mbio ashinde anapewa zawadi? Kwa hivyo mimi nilikua mmoja walipikia Mau Mau lakini sikuenda msituni lakini hawangeweza kupigana vita bila kuona mtu wakuwapikia na kwa hivyo ningeliza serikali yetu, hiyo mbio yote tulikimbia na watoto wetu wakamalizika na wakawacha vizazi vyao hapa hatujasikia mshara kwa watu hao wa pewe bonus.

Kwa hivyo nimefurahi sana kwa yule mama amezungumuza hapa kwa sababu tulipigania mashamba katika hii nchi yetu kama hii Naro Moru vijiji vinatoka wapi na tulifukuza wazungu? Kwa hivyo mashamba, tunaona watoto wakitaaibika. Ya pili ningeliza serikali yetu hivi tumezaa watoto na tumewasomesha sana na sasa wamekua crooks wakizurura town hapa ni wezi kwa sababu ya kukosa kazi. Hiyo kazi yote ya kusomesha tunafanya ya nini na hawatapata kazi. Kwa hivyo mimi nauliza serikali haina

makosa lakini ningetaka irekebishe.

Tena, watu katika bunge kwa sababu sasa tumeelekea mwaka wa uchaguzi, Mzee Kenyatta tangu afariki sijui ni miaka ngapi sasa, aliwacha Mzee Moi kijana wa rika langu hapa amemaliza miaka hiyo yote akiwa bunge pamoja na watu wake. Watoto hawa wote ambao tumewashomesha kwa nini hawaendi bunge? Wengine wanamaliza 20-30 years, nataka wamalize miaka mitano wanatoka na hao watoto wetu ambayo tunasomesha wanaingia wanakula matunda. Anavuna matunda anakula miaka hiyo mitano. Kwa hivyo mimi sitaki kukaa muda murefu kwa sababu hakuna masaa. Mimi ni mwanasiasa wa hapa Kenya na ningefurahi sana nikisika Mau Mau wamekumbukwa kwa sababu hakuna mtu ambaye hana shukrani. Sina mengi ni hayo tu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Wale wana memorandum tafadhali wapeane. Francis Mwangi?

Francis Mwangi: Thank you Mr. Commissioner Sir, I will be very brief. I am Francis Mwangi and to my points. First I think that the Vice President's office should be empowered because the Vice President in Kenya currently acts as an Assistant Minister. Second to my point, I think that the President should be elected and should not be a Member of Parliament and he should be elected through the 50% majority from five provinces.

The number of ministries should be limited to 13-15 minutes. My fourth point, I think the Members of Parliament and civic members, councillors should be accessible to the electorate. For example myself ,I do not even know my Member of Parliament and my councillor. I do not know them, so Mr. Commissioner, I think you are going to take that, that the parliamentary and civic members should be accessible to their electorate.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. That is why we are saying if an MP is not available to his own people to work with them, kuna haja yake kuwa bunge kweli? Ndio watu wengi wanasema tuwe na haki ya kuwaita hata kabla yao term ya kuisha. Tupate Mathenge Wanderi. Please, only those points that have not been discussed. Mr. Wanderi?

Mathenge Wanderi: My name is Mathenge Wanderi.

Com. Bishop Bernard Njoroge: You have a memorandum? I just want you to highlight because memorandums should be given there.

Mathenge Wanderi: I understand that. Na mimi ndiye Chairman wa Democratic Party hapa Kieni.

Kwanza ningependa kusema ile memorandum ilipeanwa na National Alliance for Change na ile ya Democratic Party from headquarters, tuliung mkono kama sub branch ya Kieni.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Just before you speak, Daniel Dothia unaweza kupeana memorandum yako? Huna memorandum. Richard Gatia? Huna memorandum. Peter Mathenge? You do not have a memorandum. Okay, fine.

Mathenge Wanderi: Thank you Commissioner. Kwa hivyo ningependa kusema ya kwanza, first and foremost the Constitution we have in Kenya today it is not bad. The problem we have is its implementation. Kwa hivyo hata hii tukitengeneza ikiwa haiwezi kufanyiwa kazi, itakua ya bure. Kwa hivyo lazima this Constitution that we are proposing must have a way of enforcing it in Parliament and when the Constitution forums meet they should come with the way through which the Government must be forced to enforce the Constitution.

The other point I would like to say is our Constitution should have a preamble which must....

Com. Bishop Bernard Njoroge: Have you written it here, is it contained in your memorandum?

Mathenge Wanderi: I am highlighting what is not there. It must involve the integrity of the people of this nation. The preamble must look at the way through which we can integrate the people of this nation.

The other important point I think I should highlight is that after the election, currently we have 210 constituencies in this country, we feel that we are not properly represented overall, to take care of these imbalances whereby kuna pahali peingine kuna watu wengi sana lakini they are not properly represented....

Com. Bishop Bernard Njoroge: Can you make suggestions.

Mathenge Wanderi: Yes. I am suggesting that during the next election we have another 100 nominated MP's all over the country and they be distributed according to the votes cast for each political party, proportionately.

The other one I would like to highlight is defence and national security. Kuna watu wengine kama mumesikia hapa vile walipigwa huko Rift Valley na pali peingine. We should have a national security advisory committee ambayo itakutana wakati wowote kuna shida kuhusu mambo ya hapa nchini kama ile tribal clashes au invasion from outside and the President being the Commander in Chief should follow the instructions of that committee.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Okay. Another point.

Mathenge Wanderi: The other one I think has been said about the Office of the Ombudsman. About political parties, any political party should have at least 100,000 registered members before it is registered so that nobody wakes up one morning and goes and registers a party and says it is a party that goes for elections. At least 100,000 registered members who must be

known and distributed countrywide.

The other one on the elections, I think it has been said about the Government, 50% of votes. The other point I would like to say is that after the election, we should have constituency kama wakina mama wote wanachagua representatives wao Parliament after the election has been done through the constituencies. We have other interest groups, women, disabled and the youth, they have specific numbers of seats allocated to them to elect representatives in Parliament.

Com. Bishop Bernard Njoroge: The last point.

Mathemge Wanderi: Not the last one.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Excuse me, I am telling you to say your last point because you have a memorandum and I have given you time to talk.

Mathenge Wanderi: Ministries should be abolished or created by Parliament not the Head of State.

Com. Bishop Bernard Njoroge: How many ministries?

Mathenge Wanderi: A maximum of 18. My last point would be any Head of State who retires from the office should be given benefits and security only if he does not continue to be active in politics. Kama the present President akitoka na anataka kuendelea kuwa Chairman wa party, he should not be given any security, any benefits and he should cease, they should be curtailed.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much that is very well said. Can we have your memorandum please. I see it is very well written and I cannot wait to read it. Can we have Peter Ndaiga? Karibu, karibu haraka.

Peter Ndaiga: Kwa jina naitwa Peter Ndaiga na Mr. Commissioner ningeshukuru na ninasema asante sana kwa nafasi hiyo. Sasa mimi ni mkaaji wa Naro Moru, tunakaa hapa Naro Moru katika town hapa tuko na...

Com. Bishop Bernard Njoroge: Mimi nataka useme maoni sitaki uniambie mahali unakaa.

Peter Ndaiga: Sasa kwa hivyo nilikua naona ni vizuri sana kukuwa hapa kwa kubadilisha Katiba kwa vile tumeonelea taabu nyingi sana tangu tupate Uhuru. Tunakaa na sheria moja ama tumekaa na sheria mbili zile ambazo hatuwezi kupindua. Sasa nimeona maoni yangu ni mazuri sana kama Katiba inaweza ikabadilishwa tukawa na nguvu ya kuongea na wakubwa wetu yaani na wale watu tumewachagua hapa katika mbunge akiwa ni President ama ni bunge ama ni councillor, tukuwe na nguvu ya

kuongea na hawa viongozi wetu.

Kwa hivyo sasa ningependa sana na nime shukuru sana na nimekuja hapa kwa kuwapa nguvu wale watu wote wanakuja tujaribu kuona Katiba imebadilishwa. Asante sana sina mengi.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Asante sana. Bila shaka Mungu atasaidia na maombi yako yatafikia. Thank you very much. Margaret Wanjira? Nimefurahi kwa kina mama kungojea.

Margaret Wanjira Gathogo: Jina langu ni Margaret Wanjira Gathogo. Asante sana Bwana Commissioner kwa sababu ya kutulete hapa Naro Moru.

Mimi kwanza maoni yangu ni mambo haya ya widows, wakina mama wale mabwana wao wamefariki. Wanapata taabu sana ya pesa kwa mfano bwana yake alikuwa ameajitiwa. Kama alikuwa mwalimu ama ameandikwa na Posta. Kama sasa cheque inapelekwa kwa DC ati inagawanywa kwa watoto. Hizo pesa zinakaa sana haisaidii watoto. Na tena hata kama zitakuja kusaidia watoto, zinagawanywa watoto zikisomesha watoto, zingine mtoto akipita aende University unasikia sasa huyo mtoto haendelei.

Kama kuna pesa zingine zilikuwa zimebaki hawakupatii ati usomeshe watoto. Kwa hivyo wakina mama wame taabika sana. Hayo mambo tunataka yabadilishwe sasa. Ati kama ni mama bwana yake amefariki, kama ni cheque pahali alikuwa ameandikwa achukuwe, cheque hiyo mama apatiwe aende akasomeshe watoto wake kama ni ya kazi afungue pahali anataka.

Tena yako mambo mengine yanasumbua wakina mama sana. Kama bwana yake amefariki wako wengine ndugu zake wanaenda kama pale ameajiriwa Nairobi kwa Head Office kama ni mwalimu ati huyo bibi ya ndugu yangu hatumjui. Tunafikiria ni rafiki yake, ati sasa hiyo pesa, question inaandikwa hapo. Huyo mama hata akienda kufuata hizo pesa, pengine mama hana pesa ya kuajii wakii ama mtu ya ku defend yeye akitafuta hizo pesa. Akienda tena ati aseme anaenda Nairobi, watu wa nymbani tena wanaanza kumdharau. Unaona sasa huyu mama anaanza kuzurura na anaenda tu kutafuta pesa za bwana yake. Hayo ni mambo mabaya sana.

Tena hilo jambo tunataka libadilishwe kabisa, hati ata kama ni baba ya bwana, akifariki kijana wake, asiende ati kuitisaha pesa ati ni ya bibi. Aseme huyu mtoto alikuwa wangu na anataka cheque ya pesa. Sijui walicana namna gani ama nini na pengine hata wako na watoto watatu ama wanne. Ati baba anaenda Nairobi head office ati anasema anaenda kusema huyo mama asipatiwe cheque ya pesa ya bwana yake ati kwa sababu huyo mtoto ni wangu.

Sasa, tunashindwa haya mambo yanatoka tena mambo ya bibi yanaenda kwa mtoto namna gani.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Mama, hiyo nimepata.

Margaret Wanjira Gathogo: Asante, hiyo nimemaliza. Ile ingine ni mambo ya pombe. Tuna onelea sisi kama wazazi sasa, watoto wameharibika sana na pombe na serikali mbeleni ilikuwa imeweka masaa za pombe. Siku hizi hakuna. Tungependelea kama sisi wazazi na sana sana wakina mama kwa sababu hata wale wameandikwa wana taabika sana. Pombe huwachwa kuanzia ashubhi mpaka asubhui ile nyingine ati hakuna mtu anauliza. Wacha watu wakunywe pombe kuanzia saa nane mpaka saa tisa ya usiku ndio watu waende wakalale hata wale wanafanya kazi huko.

Hiyo nyingine ya tatu ni habari ya government workers. Watu wanandikwa na serikali wakiwa retired hata cheque zao, kwanza cheque zao wapatiwe saa hizo vile hanaanza kuandika retirement letter hata cheque zao waende nazo hakuna mambo ya kungojea ati miezi tatu, ya nini na barua ulinipatia ati retire? Apatiwe benefits zake zote aende akapumzike na mambo yake yote. Hakuna ati kurudi kuenda Nairobi kutafuta mtu ati amsaidie apatiane elfu tano. Hakuna, hatutaki hiyo.

Ya nne nayo ni ya watoto chokora. Watoto hawa chokora tunataka hii Katiba ibadilishe ifanye hii kazi ziwe ya serikali. Watoto wasomeshwe wote. Wanaweza kuwa madaktari, wanaweza kuwa hata army ama police. Wawe watu wa kutumikia raia wengine ama serikali. Vile mtoto anaweza kusoma pia iwe responsibility ya serikali lakini si ya mtu ama nani ama tuseme ni hawa wamefanya vibaya. Hatutaki, serikali iwachukuwe watoto wote iwajengee mashule.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Margaret ya mwisho.

Margaret Wanjira Gathogo: Hii ya mwisho nayo ni Chiefs na Assistant Chief. Wawe wakichaguliwa na raia ili kama watu wamekaa kama miaka kumi, ishirini, na wengine hawawasaidii raia vizuri na kwa sababu si raia waliwachaguwa, wanafanya kazi mbaya sana. Tungetaka sasa tuwachaguwe ili wakikaa kama ni miaka tatu ama nne, tuwatoe tuweke wengine. Hata councillors, hata MP namna hiyo kwa sababu wanakaa hapo miaka mitano. Lakini tukiona ni mbaya kwa miaka miwili, ya tatu tunachagua tupatiwe ruhusa ya kuchagua mwengine aendelea na kazi badala ya kulala hapo miaka kumi, miaka ishirini. Kwanza wakina mama wanateseka sana. Asante sana.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you mama. Margaret, those are very good suggestions. Nikiona wakina mama wakizungumuza hivyo nasikia furaha. Peter Mathenge Gitonga. You are Peter Gitonga? Please Peter, we would like you to mention only those points that have not been discussed. Do you have a memorandum?

Peter Mathenge Gitonga: I do not have a memorandum.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Is that well written?

Peter Mathenge Gitonga: It is not well written it is just points that I will just highlight.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Because we would like to take it don't mind because we can read it.

Peter Mathenge Gitonga: These are just like my notes. Kwa jina mimi naitwa Mathenge Gitonga. Mimi ni mkaazi wa Kieni Constituency na niko na haya ya kusema kuhusu marekebisho ya Katiba.

Ningependelea kama ile Katiba tutaiunda itakuwa iko na maneno fulani kuhusu transition. Moja ni tarehe ya uchaguzi iko certain.

It is not the President who is going to fix the date of the General Elections. Ningependelea bunge iwe na calendar yake na Rais asiwe na power ya ku-dissolve Parliament.

Pia uchaguzi ukifanywa ningependelea kuwe kuna ile tarehe ambayo Rais mpya ataopishwa kama vile huko America, a specific date and a specific place so that we are certain. Hatutaki kusikia mtu aliapishwa asubhui kama ameiba uchaguzi kwake nyumbani.

Tena ningependelea kabla ya uchaguzi ambao pengine tunaweza kufanya ama ile itafanywa, constituencies ziwe reviewed kwa sababu wale wako bunge, wako bunge kuwakilisha wananchi, hawako huko kuakilisha land mass. Wale wako, wengine wamepelekwa huko na wananchi wachache. Hizo constituencies ziwe merged na zile kubwa sana ambazo haziwezi kuwa effectively represented na mbunge mmoja zigawanywe kabla ya uchaguzi.

Com. Bishop Bernard Njoroge: What population would you prefer for constituencies?

Peter Mathenge Gitonga: What population in a constituency? A constituency should not have more than 40,000 registered voters. We now have some constituencies with about 7 or 8 thousand people.

Pia ningependelea katika political parties, kama chama kiko na asili mia kumi ya wabunge ikuwe funded na serikali. Vyama vingine ambavyo vimekuwa registered na havina members visi- qualify kuingia kwa ballot paper kwa sababu wakati vinaingia kwa ballot paper vinaifanya ikuwe complicated sana na inakuwa shida hata wakati wa uchaguzi.

Pia ningependelea vikosi vyote vya wanajeshi au all Armed Forces wawe wamewekwa kwa Katiba na kazi yao imekuwa set out properly. Tusikuwe na watu waki-form vikosi vingine ambavyo ni vya halali wakisema ni Mungiki, ni Kamjesh na vingine ambavyo vinahatarisha wananchi.

Pia ningependelea kama vikosi vya Police na especially kama ni za Special Branch kuwe na sheria haviwezi kutumiwa vibaya

kuhujumu nchi. Vitumiwe vizuri kuhusu intelligence gathering methods za economic social issues ambazo zinaweza kusaidia wananchi lakini sio siasa tu ya ku-protect wale wenye wamekalia viti wakati huu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Can we have the last point?

Peter Mathenge Gitonga: The last point I think has been said before, that is ningependelea wale ma-officers wamechaguliwa na serikali kwa viti vya juu kama ma-Judge, kama Permanent Secretaries, Managing Directors wa public corporations wakuwe vetted na Parliament na wasichaguliwe na mtu moja tu ambaye anaweza kuwachagua wale ambao hawahitaji, hawastahili kupata hivyo viti.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. You have given us very good ideas but I do not mind taking that with me, it is okay.

Peter Mathenge Gitonga: I promise to deliver a memorandum in your offices.

Com. Bishop Bernard Njoroge: In Kencom House? Fine, ask for Com. Bishop Bernard Njoroge, I will be happy. Eliud Kanubi? Unitwa Kanubi Gatiki? Uko na jina ngapi? Jackson Muchemi?

Jackson Muchemi: Asante sana. Majina yangu naitwa Jackson Muchemi na ni machache tuu ambayo yale mimi naweza kuongea kwa sababu mengine yameshaongewa na wenzangu wale walikuwa hapa mbeleni.

Kwa hivyo yale mimi nataka kuongea ni machache tu, mawili tu yafuatayo. Ya kwanza ni habari ya wafanyakazi wa serikali kama Chiefs na manaibu wao. Hawa Cheifs na manaibu wao, hawa ndio watu wale ambao wanajua masilahi ya wananchi huko nyumbani na ndio wanakaa na wananchi sana na ndio wanzjua taabu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Ungetaka nini juu yao?

Jackson Muchemi: Ningetaka, sababu kuna sheria ilikuweco hapo kitambo ya Chiefs na ya manaibu wao na ikaondolewa, ningetaka irudishwe. Ya pili ni habari ya misitu. Habari ya misitu naye imeshakuwa mbaya sana kwa sababu wale watu walikuwa wakifanya kazi kwa misitu waliondolewa sasa kazi ikapewa watu wa KWS kama kwa Mt. Kenya. Na sasa huko hakuna maendeleo inaonekana ya kupanda miti ya kutumia au kufanya nini kwa sababu hawa watu wa KWS hawajui habari ya miti wanajuwa tu habari ya wanyama. Ningependelea warudishwe hao watu walikuwa wanafanya kazi kwa misitu ndio wafanye kazi ndio tupate kuwa na misitu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Haya, nyingine.

Jackson Muchemi: Ya tatu ni habari ya mazao ya wananchi kwa sababu serikali haishughuliki na yale mazao wananchi wanafanya, wanalima huko mashambani. Ningependelea hii serikali iweke habari ya mazao ya wananchi kujua itauzwa namna gani na wananchi watagawiwa namna gani kama vile wanaweka habari ya majani au kahawa kwa sababu hata wakulima hawa wengine wana taabu kwa hiyo mimea yao, kwa chakula chao ambacho wanalima. Serikali ishughulikie hawa watu. Asante sana.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Asante. Thank you umesema maneno makubwa ya maana na tutaangalia. John Maina? Usirudie yale yamesemwa.

John Maina: My name is John Maina, I am from Naro Moru and I am a student. My first point is the freedom of worship. This Act should be amended or should be rescinded to avoid the confusion or the up-coming problems such as the rising of devil worship and some cults which breed problems and commotion in the society.

Second point; Free and compulsory education. Primary education should be provided freely, this can be enhanced by; one, by reducing the MP's and the President's allowances.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Now, if you say free and compulsory education that will be taken care of. They can find other ways to get money.

John Maina: Okay. The third is strengthening of our national language. Kiswahili language should be enhanced and should be encouraged to enhance national unity amongst people in the society.

The fourth point is awarding of freedom fighters. Five, currency; if the current President comes out of power the currency should retain his photo, the photo should remain. The sixth point is the enforcement of the Constitution as per what is stated. Seventh point is the creation of national security advisory council to enhance security in the nation to avoid commotion and problems in the society. The eighth point is the implementation of Chief's Act. Since Chief and Assistant Chief know people's problems and are much acquainted with the problems they are able to help people and to listen to their grievances.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much you have said very important things. Rachael Muthoni?

Rachael Muthoni: Mimi naitwa Rachel Muthoni Murage. Maoni yangu, nasema Kiswahili kitumike katika mahakama. Mambo ya kupewa hati ya mashamba irahisishwe bila rushwa. Pia Polisi wafanye kazi bila rushwa. Atakaye patikana akipewa rushwa ashtakiwe na aondolewa kazini. Katiba iangalie wajane. Watu ambayo hawawezi kuajii mawakili wasaidiwe na serikali.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. Unajua mtu anaweza kusema maneno makubwa sana na yawe ni machache. Thank you very much Rachel. Priscilla Wanjiru? Wakina mama mumejaribu mumekaa mpaka mwisho. Karibu hapa Priscilla. I am very proud of you.

Priscilla Wanjiru: Jina langu ni Priscilla Wanjiru. Kile nataka kusema ni kwamba tulipigania uhuru na tulipigana kwa sababu tulikuwa tunataka watoto wetu wapate matunda ya uhuru na wakati watoto wetu walisoma na kumaliza hawapati ajia ama kazi.

Ya pili yenye nataka kusema ni kwamba mama maskini ananyang'anywa shamba na matajiri na wakati huo akinyang'anywa, case yake ikipelekwa kotini inachukuliwa kama ya mtu maskini sio kama ya tajiri. Maneno haya tungetaka yashughulikiwe na court kama inavyostahili. Na watoto wetu nao wapatiwe ajia.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you muno Priscilla niodo wa shiugo ishio wauga nigo kinya. Niwega mno todo ni kama tumemaliza wale watu wote waliotaka kuzungumuza leo na ikiwa kuna mmoja ambaye haja sikia jina lake aje hapa mbele. Kwanza tuanze na wewe na uniambie jina lako.

Eliud Gatiki: Kwa jina mimi ni Eliud Gatiki kutoka hapa Kaburaini sub location.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Eliud who? Gatiki.

Eliud Gatiki: Ya kwanza free education kutoka Standard 1 mpaka Form 4. Kama mtu akipita Form 4, irudiwe vile ilikuwa ya zamani, Form 6 unafanya mtihani halafu unaingia University. Hiyo education ikuwe namna hiyo.

Ile ingine, free medical attention. Kila mtu asaidiwe kwa sababu sisi watu wale tunakaa hapa rural hatuna pesa tunapata. Tunateseka sana kwa ugonjwa wana kufa bure na hatuna usaidizi. Ya tatu sasa tunakuja hapa kama kulete maoni yetu. Sasa uko ugonjwa unamaliza watu na kama iko Commission na watu hawajasomeshwa kuhusu hii ugonjwa, hii itakua ya bure. Watu watakwisha na munataka mambo yote yageuzwe. Maoni yangu ni serikali kwanza ifanye hii, ili watu waokoke au wasikufe wote.

Ile ingine ni mashamba yale yako na wazungu na watu weusi. Wako na ma shamba kubwa na watu wanakaa kwa vijiji. Mimi naonelea ile shamba ceiling ipatiwe ya acre mia moja au elfu moja. Ile mengine yauziwe wananchi waone mahali pa kufanya kazi kwa sababu watu wengi wanakaa kwa vijiji na hakuna pa kulima.

Ile ingine, tunataka hao watu, vijana, kuwe na viwanda vingi vy kufanyia kazi kwa sababu watoto wetu wote wanasoma tunakaa nao, wanakua kama refugees. Tuko nao nyumbani, hakuna mahali pa kwenda. Wanatusumbua, na kama kukiwa na

viwanda vingi, hao watoto watakwenda kufanya kazi, kila mtu atapata riziki yake. Tungetaka hayo.

Ile ingine ya mwisho. Tungetaka serikali ile itakuja baadaye ione kwamba kila kitu wanafanya huko bunge na ile bunge isiwe bunge ya ukabila iwe bunge ya watu wote kwa sababu wakati wa kuchagua, hakuna ukabila. Na kama wanaingina huko, ukabila unaingia. Tunataka bunge isio na ukabila ili nchi yetu iendelee. Asante sana Bwana Commissioner.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. Haiya mzee, na wewe njoo na utuambie jina lako.

Erastus Nderitu: Jina langu ni Erastus Nderitu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Okay, Erastus who?

Erastus Nderitu: Nderitu Gathioni. I would like to bring my contribution to this Commission. One, the Government should have the responsibility to care for all Kenyans and let them enjoy their rights. Kenya should have access to information in possession of the State. Wives and all children should have a right to inherit land from their families. We should have a congress to control the executives, the finances and human resources and it should remain with the Parliament. Sales tax should be abolished and poll tax introduced where every adult will have to pay every month. This will be controlled by the County Council or Local Authority.

The Public Service Commission should be free and impartial. Members of the Commission should be vetted by Parliament and enjoy security of tenure. It should retain power to where required including all other indisiplined cases are in the Civil Service.

Code of regulation should be reintroduced and every civil servant made to read it and understand on appointment and those still in service provided. They should declare their assets. All natural resources should be protected by the Government and even authorised by the Local Authority. This will give the people who are near the various forests and the like, to have the cake of what is being produced from those forests.

The senior citizens, most elderly people who have retired from Government services, should be taken care of by the Government. Their purchasing powers should be used or increased by their pension package and whenever civil servants salaries are increased, should be increased as well. Thank you Mr. Commissioner.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. Pension package should be increased with the increase of salary. Okay, kuna mtu mwingine yeyote? Haya, wewe njoo hapa na ndio wa mwisho, utuambie jina lako.

Stephen Munga: Kwa majina mimi ni Stephen Munga. Yangu ya kwanza ninaonelea ni kuhusu kazi. Kila mtu anatakikana

afanye kazi ndio aweze kuishi lakini unakuta mtu mmoja ako na kazi zaidi ya ishirini. Unakuta mtu ako ni yale magari kuu kuu kwa barabara tena ndiye huyo mtu anakujaa kuweka kinyozi kwa center kidogo kama hapa Naro Moru. Tena ako na shamba analima, ako na kazi nyingine ya kuchunga mbuzi. Sasa inakuwa wananchi wanaishi kwa ukahaba kwa kuwa kazi zote ziko na wale watu wako na pesa. Wanachukua kazi nyingi, alafu wanaajii hawa watu wadogo wadogo kwa mshahara kidogo.

Ile ingine ni kuhusu hizi case zinachukuliwa na mawakili. Mtu wako akigongwa na gari anakuonyesha vile atakwenda na atakusimamia. Wakati wa malipo hizo pesa zikifikia kwake, inakuwa ni ngumu kuzipata kutoka kwake. Sasa mimi nilikuwa naonelea ni heri hizo pesa zipatiwe mwenye ajali au mtu claimant wa hiyo ajali kuliko wakili kwa sababu wakili anajua vile atakuitisha hizo pesa achukuwe zake. Kuliko yeye mwenyewe achukuwe hizo pesa tena inakuwa ni ngumu kumfuata. Hayo ndio maoni yangu.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Thank you very much. Tunakushukuru sana kwa hayo maoni. Bila shaka yatafika mahali yanahitaji. Ningetaka kushukuru nyinyi nyote ambao mumekuja leo. Nafikiri tumekuwa na zaidi ya watu mia moja ambayo ni watu wengi sana kusikiza.

Pili ningetaka kushukuru kwa sababu maoni yenu yalikuwa na mwelekeo. Mumetoa maneno mengine ambayo sikuwa nimeisikia. Nilikuwa huko Karatina, nilikuwa Kirinyaga, nimekua Gatundu, nimekua kila mahali lakini nimependezwa sana na maoni yenu. Na zaidi nimependezwa na akina mama. Wametoa maneno mazuri, wamekaa mpaka mwisho kwa hivyo ninashukuru Mungu kwaajili yenu nyinyi wakina mama.

Ningetaka kumalizia kwa kusema tusife moyo. Kweli tumekuwa na taabu lakini pia Mungu naye ametusikia. Labda kwa njia hii Kenya itakuwa nchi mpya na haya mambo tunazungumza ya kukosa kazi, ya wazee kukosa mtu wa kuwatunza, shida kujaa kila mahali, mimi nina tumaini kwamba katika Katiba hii na wale watakao kuja kutawala chini ya Katiba hii mpya, mambo yatakuwa tafauti. Pia tunahitaji tukumbuke Mungu na tuishi maisha inalingana na yale tunasema katika dini hii. Naturudie mambo yetu ya kale yale yalituweka ili ituweke kama watu, si ni kweli? Na tujali kila mtu na jaama yake na tukiwa na watu walio na taabu wanaoishi karibu na sisi, tunajaribu kuwatunza.

Mungu ametusahau kwa sababu kitu tumefanya hivi, siku hizi ni kujipenda sana. Kila mtu anapenda mambo yake na huwezi kumfikiria jirani yako hata kama ni disabled, huna haja na yeye na hayo tunazidi kujiua sisi wenyewe. Kwa hivyo tuwe na matumaini. Watu wasio na matumaini hawana maisha, maisha yanaletwa na matumaini. Tuseme kesho mambo yanaweza kubadilika na katika Katiba mpya, tutakuwa watu wapya na nchi mpya. Hii ni nchi nzuri. Tuntumaini siku moja hakuna mtu atakaa bila shamba na tuna tumaini siku moja katika Katiba hii itaeleza kwamba huwezi kupata zaidi ya kiwango hiki cha shamba na hakuna mtu ambaye atakaa katika barabara tukiwa tuko nchi moja.

Na mwisho, mambo haya yote mwishowe tutayaacha si ni kweli? Lakini tukienda kutengeneza Katiba muwe na ushuhuda huu

kwamba munaweza kuamini Commission hii ya kwamba mwishoe itakuja na Katiba ambayo itachukua masilahi yenu. Ningaetaka kujua kama civic education providers wako hapa. We want to recognize them mukisimama. Thank you very much for the work you have done. I want to recognize that work, na kazi yenu haijaisha, nina tumaini Katiba hii ikimalizika, tutakuwa na zaidi ya miaka mitatu ya kuwafundisha watu. Na hata ingawa ni kujitoka, hakuna pesa, lakini hakuna kazi nzuri mtu anayofanya ambayo haitalipwa. I believe that. Sawa Sawa.

Now, 3 C's wako wapi? 3 C's pia wasimame. Okay. I just want to thank you na muambie wale wengine tumeshukuru tumeona kwamba mulikuwa mumeifanya kazi na kazi yenu imeonekana na maoni ambayo yametolewa. Kwa hivyo Mungu awabariki pia nitasema hata nyinyi, bilashaka mtalipwa. Sijui kama Programme Officer analolote alafu kama hana tunaweza kuomba na tumalize hiki kikao. Kuna kitu ungetaka kusema? You do not see them. Is that so, maybe they have been somewhere else. Mugo, what we want is civic educators wa hapa. Huyu anasema haja waona. Muulize anakaa wapi.

Speaker: Most of the times we go to the churches, we go to where people have assembled but many times we ask people to wait for civic education and they do not wait. Tumesha enda kwa PCEA, tumeenda kwa CPK na nafurahi kwa sababu watu wa CPK wametoa maoni kama vile tuliongoza hawa na watu ya PCEA. Lakini watu wengine wakisikia iko civic education hawajali. Kwa hivyo sote tujali kwa sababu kutengeneza Kenya ni jukumu letu sote. Mtu akisikia kuna civic education pahali popote tafadhali karibia halafu utaelemishwa vile pengine unaweza kuendesha nchi yako. Asanteni.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Asante sana. Ningetaka kumuuliza, kuna Muislamu hapa? Okay, ningetaka kuuliza huyu mukorino aje aombe. Wewe ulinaambia ni Chief?

Absolom Mwangi: Mimi ni mtumishi wa Mungu na mimi ni area chairman wa Naro Moru sub location na nimewakaribisha nyinyi sana katika kikao hiki.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Ngoja kuna mtu ana mkono pale. Okay.

Speaker: Ninaona tumefanya kazi kubwa sana ya kufanya Katiba mpya. Katiba ilioko sasa ni lazima President aweke sahihi ndio iwe sheria. Nauliza, mukimaliza kazi yenu, ni lazima itaenda huko ndio iwe sheria au muna right, yaani vile tumesema ikiwa sheria ni nyinyi mutapitisha bila kuenda mahali pengine?

Com. Bishop Bernard Njoroge: Sijui kama ulikuwa hapa wakati nilieleza vile itapitishwa. Lakini unajua tukitaka kuwa na transition nzuri ni lazima tufuate sheria. Ile Katiba ilioko inasema kwamba ni lazima Katiba hii mwishowe ipelekwe bunge. Hatutaki kuharibu sheria, si ni kweli? Kwa sababu tukiharibu hii iko na ile nyingine itaharibiwa. Lakini kupelekwa bunge haitazungumzwa na wabunge kwas ababu tayari watakwua wameizungumzia katika National Conference. Si ndivyo niliwambia? Yao tu nikupiga nini? Muhuri, ionekane kwamba imepitia wapi? Parliament. Naye President, hii ikipitishwa na

National Conference, yake tu nkuweka nini? Kidole. Hana jukumu lingine na hawezi kukata kuweka nini? Kidole. Kwa sababu hiyo ni sheria. Akikataa sheria nayo itamshika unasikia? Na kuna sheria nyingine ambaye ni ngumu hata kuliko ya karatasi. Sheria hii, kwamba hii Katiba imetengenezwa na watu wote wa Kenya, nani anaweza kuchezea uzito wa watu? Kuna mtu anaweza? Hii itakua ni ngumu sana na ndiyo unaona hata wale wanaotawala wanaogopa kwas ababu si ni watu walisema wanataka Katiba? Si ni kweli? Wakaenda kwa streets wakasema wanataka iwe people driven. Si ndio tuko hapa? Hii haikutokana na wanasiasa, imetokana na nini? Wanainchi?

Unawajua watu ni kama mvua, mvua ikinyesha kwa siku mbili unaweza kutembea kwa huyo maji? Yatakupeleka. Na katika Katiba, watu ni kama mvua na mtu yeyote akisimama katika hiyo Katiba atafanya nini? Sawa sawa, ume sikia hivyo. Haya, njoo hapa mchuganji utuombe.

Absolom Mwangi: Nigeomba wale watu ambao wako na kofia na wakiwa katika jumba hili waweke kofia chini ili tumheshimu Mwenyezi Mungu. Ningependa kushukuru hawa wazee na makarani wale ambao wamefika katika sub location yangu ya Naro Moro\u siku hii ya leo kwa ajili ya siku hii ya Katiba. Na hsukuru mazee wetu wa Commission na watu wake wote na tunawaomba safari njema wakirudi kwao mutukumbuke Naro Moru siku nyingine na tunawakaribisha katika kikao hiki. Kikao hiki kina Chief wake ambaye ni Elijah Waititu na Assistant Chief wake Bwana Paul Kangora na mimi nigeconda kama mchungaji wa Mungu Absolom Mwangi Migiwe nataka kushukuru Bwana Kinyua ambaye hii ushubhi ya leo alinikaribisha katika kikao hiki.

Mimi nilikuwa naenda kutafuta mboga kwa ajili ya watoto wangu lakini Bwana Kinyua akanihimiza kabisa akaniambia ewe rudi tumekuja kwako siku ya leo, Kwa hivyo mimi nikakuja hapa na ndio mimi nimekuwa hapa. Sasa nataka twende kwa maombi kwa Mwenyezi Mungu katika siku hii ya leo. Tujiweke tayari katika siku hii ya leo. Sio kujiwake tuu tayari kwa Katiba, hata kwa roho zetu sisi tuziweke tayari tukijua kwamba sisi ni wasafiri hapa duniani na siku moja Bwana Yesu Kristu anatuambia katika maandiko yake John kumi na nne, alienda kutuandalia dhalla mahali na sisi siku moja tutakuwa katika kikao hicho. Mimi na wewe, tu jiweke tayari katika safari ya kutoka hapa duniani kuenda mbinguni. Naanza maombi.

Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe ufalme wako uje, mapenzi yako yatendeke humu duniani kama ambavyo yanatendeka mbinguni. Utupe hicho chakula chetu cha kututosha, utu samehe makosa yetu kama sisi tunavyo samehe wale ambao wanatukosea, usitupeleke majaribuni bali utuokoe katika yale maovu na tunaomba hayo machache kwa jina lako na la Yesu Kristu mwanao. Tunomba na kuamini sote tunasema Amen.

Wale ambao wanakwenda nendeni safari njema na Mungu awaongoze tukutane tena.

Com. Bishop Bernard Njoroge: Ningetaka kumubariki na kufurahia Father wa Catholic hii, wa Parish hii kwa ajili ya kuturuhusu kutumia mahali hapa. Tunashukuru sana na mzee wa kanisa mwambie tumefurahia na Mungu amubariki. Asante.

